Toleo 90 - Dhu al-Hijjah 1445 H / Julai 2024 M

# Jarida la UQAB

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Sera za Kifedha za Kibepari hazina Maadili na Ubinadamu

**HABARI NA MAONI**
Chochote Kinacholevya Ni Tembo Na Kila Tembo Ni Haramu

**MATOLEO**
Marufuku ya Hijab ya Ubelgiji: Kutopendelea upande wowote kama Haki mpya ya Kimungu (Droit Divin)

**JIBU LA SWALI**
Uhalisia wa Hizb ut Tahrir Baada ya Kusimamishwa Khilafah



**Afisi ya Habari Kenya**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿ وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ
الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا
يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ﴾

حزب التحرير
HIZB UT TAHRIR

KUMB: 17/1445 | Ijumaa, 15 Dhu al-Hijjah 1445 H | 21/06/2024 M

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Sera za Kifedha za Kibepari hazina Maadili na Ubinadamu

Maandamano ya Kupinga Mswada wa Fedha nchini Kenya yameenea kutoka mji mkuu Nairobi hadi sehemu mbalimbali za nchi, huku walipa kodi wakiendelea kupinga mpango wa Rais William Ruto wa kufadhili Bajeti yake ya Ksh3.9 trilioni (dolari bilioni 31). Mnamo siku ya Alhamisi asubuhi, maandamano ya barabarani yaliregea katika barabara za Nairobi baada ya mapumziko ya saa 24, huku polisi waliokuwa wamejihami wakifyatua vitoa machozi kuwatawanya waandamanaji.

**Hizb ut Tahrir / Kenya ingependa kuangazia yafuatayo:**

Bajeti na sheria za kifedha katika tawala za Kidemokrasia ni mazao ya mfumo mbovu wa Ubepari ambao unaasisi mfumo wa fedha uliojengwa juu ya riba na kusababisha mapovu na mizigo mikubwa ya mikopo pamoja na kupanda kwa kiwango cha deni. Ili nchi yoyote ya ulimwengu wa tatu kama Kenya ibaki kuwa taifa linalostahili kupata mikopo, IMF na Benki ya Dunia (taasisi za kikoloni za Magharibi) huitisha hatua kali za kubana matumizi na sera za juu za kifedha. Zaidi ya hayo, tawala za kibepari zinategemea sana ukopaji fedha huku ubwana wa serikali ukiwa kama dhamana ya kufadhili miradi ya serikali. Hata hivyo miradi hii inakabiliwa na ufisadi na ulafi wa viongozi wa serikali hivyo kiasi kikubwa cha fedha huporwa.

Makadirio ya sasa ya bajeti yanayofikia dolari bilioni 31 pamoja na mswada wa fedha unaonyesha maumbile yasiyo ya kimaadili ya siasa ya uchumi ya ubepari ambao huvua sera hiyo kutoka kwa data za takwimu bila ubinadamu. Ni muhimu kutaja kwamba sera zote za kifedha katika uchumi huria wa Kibepari hazina maadili na ubinadamu. Pato la Taifa kwa kila Mwananchi nchini Kenya linatarajiwa kufikia Dolari za Marekani 1865.00 kufikia mwisho wa 2024, kulingana na miundo ya kimataifa ya Uchumi wa Biashara na matarajio ya wachambuzi. Katika kipindi cha muda mrefu, Pato la Taifa la Kenya kwa kila mwananchi linatarajiwa kuimarika karibu dolari za Kimarekani 1973.00 mwaka wa 2025 na Dolari za Marekani 2098.00 mwaka wa 2026. Kulingana na data hii, hali ya kiuchumi na kifedha ya raia wa kawaida imechorwa kuwa 'imara'. Ukweli wa maandamamo yaliyoenea, unathibitisha zaidi uongo wa nadharia ya mtiririko wa uchumi. (Mkono usioonekana) utajiri ukikusanywa mikononi mwa 1%.

Suluhisho msingi la masaibu ya kiuchumi nchini Kenya na duniani kwa jumla halitapatikana kupitia maandamano, badala yake, kupambana kwa ajili ya mfumo unaowachunga watu ipasavyo na kuwatendea wema. Mfumo unaomridhisha Mola wa wanadamu na kuamiliana nao kwa uadilifu kupitia kwa Ahkam (hukmu) za Uislamu. Mfumo ambao utaifanya dola yake Khilafah kuwa huru kiuchumi na kisiasa bila kuegemea zana za kiuchumi za kikoloni za ubeberu wa Magharibi.

Dola ya Khilafah, ambayo kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu (swt) kusimamishwa kwake tena kunakaribia zaidi siku baada ya siku, haitapoteza muda katika mahusiano ya umma kuandaa sheria za fedha kila mwaka. Mapato na matumizi yameteremshwa na kusuluhishwa na Mwenyezi Mungu kiwahyi, yaani, sekta zake katika bajeti ya Dola ya Khilafah huamuliwa na hukmu za kudumu za Sharia. Khilafah ina mapato aina mbalimbali kama vile Al-Ghana'im (ngawira za vita), Kharaj (kodi ya ardhi), Fai (ngawira zisizo za vita), na ushuru wa Jizya kutoka kwa wanaume wenye uwezo wasio Waislamu. Katika suala hili, Khilafah haitatoza kodi za adhabu kwa watu. Baada ya kusimamishwa tena, Khilafah itawakomboa watu duniani kutokana na udhalimu wa kupindukia na umaskini uliokithiri kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir Kenya**

# Baraza la Usalama liko “Mfukoni mwa Marekani” Likiendeshwa na Maslahi yake na Maslahi ya Mayahudi na Wakoloni wa Makafiri

Mnamo tarehe 11/6/2024, Baraza la Usalama lilitoa azimio la kuunga mkono mradi wa Biden kwa ajili uvamizi wa kikatili wa Kiyahudi dhidi ya Gaza, bali Palestina yote! Maandishi ya azimio hilo, kama yalivyochapishwa na CNN, mnamo tarehe 11 Juni 2024, yalisema yafuatayo: (Baraza la Usalama “linakaribisha pendekezo jipya la kusitisha mapigano lililotangazwa mnamo Mei 31, ambalo lilikubaliwa na ‘Israel,’ na kutoa wito kwa Hamas pia kulikubali, na kuzitaka pande husika zikubali kutekeleza masharti yake kikamilifu bila kuchelewa na bila masharti.”

Ama kuhusu pendekezo la kusitisha mapigano ambalo azimio hilo linakusudia, ni yale ambayo Rais wa Marekani Biden alikuwa ametangaza mnamo 31/5/2024 katika Ikulu ya White House, ilisema, kama ilivyotajwa na tovuti ya arabic.rt.com mnamo 1/6/2024:

[(...Sasa, baada ya diplomasia ya kina, iliyofanywa na timu yangu, mazungumzo yangu mengi na viongozi wa 'Israel', Qatar na Misri, na nchi nyingine za Mashariki ya Kati, 'Israel' sasa imetoa pendekezo kubwa jipya ... Pendekezo hili jipya lina awamu tatu:

1-**Awamu ya kwanza itadumu kwa wiki sita ambayo ingejumuisha:** Usitishaji kamili wa mapigano, uondoaji wa vikosi vya 'Israel' kutoka maeneo yote ya Gaza yenye wakaazi … Wakati wa wiki sita za awamu ya kwanza, 'Israel' na Hamas watajadiliana kuhusu mipango muhimu kufikia awamu ya pili, ambayo ni kumalizwa kwa kudumu kwa uhasama. Lakini… ikiwa mazungumzo yatachukua muda wa zaidi ya wiki sita kutoka awamu ya kwanza, usitishaji vita bado utaendelea maadamu mazungumzo yanaendelea…Marekani, Misri na Qatar zitafanya kazi kuhakikisha mazungumzo yanaendelea, hadi makubaliano yote yafikiwe.

2- **Awamu ya pili,** ambayo itajumuisha: Kuachiliwa huru kwa mateka wote waliobaki hai, wakiwemo wanajeshi wa kiume... Na maadamu Hamas itatimiza ahadi zake, usitishaji wa muda wa mapigano utakuwa, kwa maneno ya pendekezo la ‘Israel’, “kumalizwa kwa uhasama daima” ikiwa Hamas itashindwa kutimiza ahadi chini ya makubaliano hayo, 'Israel' inaweza kuregelea tena operesheni za kijeshi.

3- **Hatua ya tatu** ambapo mpango mkubwa wa ujenzi mpya wa Gaza ungeanza.)

**Biden anamalizia kwa kusema:** (- “Hivyo, nimehimiza uongozi nchini ‘Israel’ kusimama nyuma ya makubaliano haya, licha ya shinikizo lolote linalokuja.

- Na kwa watu wa ‘Israel’, acha niseme hivi. Kama mtu ambaye amekuwa na ahadi ya maisha yote kwa 'Israel,' kama rais pekee wa Marekani ambaye amewahi kwenda 'Israel' wakati wa vita, kama mtu ambaye ametuma Vikosi vya Marekani kuilinda moja kwa moja 'Israel' iliposhambuliwa na Iran, nakuombeni murudi nyuma na mufikirie kitakachotokea ikiwa wakati huu utapotezwa”.

- Na kwa mkataba huu, 'Israel' inaweza kuoanishwa kwa kina zaidi ndani ya eneo hilo, ikiwa ni pamoja na -- haishangazi kabisa, ikiwa ni pamoja na wanaojua makubaliano ya kihistoria ya uhalalishaji mahusiano na Saudi Arabia ...)]

Kinachoonekana wazi kutokana na tangazo hili ni kwamba limejaa mabomu yanayosubiri muda kulepuka ili kurefusha muda wa uvamizi. Hatoi wito wa kujiondoa kabisa, bali wa **“kuondolewa kwa majeshi ya 'Israel' kutoka maeneo yote yenye wakaazi ya Gaza...”,** na anacheza na maneno ya kudanganya na kukwepa, akisema, “Usitishaji vita kamili na wa kina... **kumaliza kwa kudumu kwa uhasama...”,** kisha anasema, **‘Ikiwa Hamas itashindwa kutimiza ahadi zake chini ya makubaliano hayo, 'Israel' inaweza kuanzisha tena operesheni za kijeshi”** na anamalizia kwa kutangaza kwamba yeye na Mayahudi wanaoikalia kwa mabavu Palestina ni wawili katika karne isiyoweza kutenganishwa. Anasema, **“Kama mtu aliye na ahadi ya maisha yote kwa 'Israeli',”** na anawatangazia juu ya uhalalishaji mahusiano wa kihistoria! “'Israel' itaweza kupata uoanishwaji zaidi katika eneo hili na mpango huu, ikiwa ni pamoja na kupitia makubaliano ya kihistoria ya uhalalisha mahusiano na Ufalme wa Saudi Arabia.” Kisha anajingonganisha mwenyewe katika uamuzi huo na kusema: **“'Israel' imewasilisha pendekezo jipya,”** yaani, kana kwamba ni pendekezo la 'Waisrael', kisha anarudi na kusema, “Nimeuhimiza uongozi wa 'Israel' kuunga mkono mkataba huu...” kana kwamba sio pendekezo la 'Israeli'! Hatimaye, licha ya umbile baya la tangazo la Biden, anasisitiza kwamba Misri na Qatar zitadhamini utekelezwaji wake pamoja na Marekani! **“Marekani, Misri na Qatar zitafanya kazi kuhakikisha mazungumzo yanaendelea hadi makubaliano yote yafikiwe.**

Uamuzi huu unajiri kufuatia mauaji ya kutisha yaliyofanywa na umbile halifu la Kiyahudi mnamo tarehe 9 Juni 2024 katika kambi ya Nuseirat, ambapo Wapalestina 274 waliuawa shahidi na wengine 698 kujeruhiwa, ambayo inawakilisha moja ya siku za umwagaji damu zaidi kwa miezi kwa watu mjini Gaza.

***Endelea... UK 4***

**Enyi Waislamu:** Si ajabu kwamba Marekani, makafiri wa kikoloni na miundo yao, dola ya Kiyahudi, wanatushambulia. Ni maadui wa Uislamu na Waislamu, sio kuanzia leo bali wa miaka mingi iliyopita. Wala si ajabu kwamba makafiri wakoloni kwa kuegemea sheria za kimataifa wanaweza kuzishambulia nchi za Kiislamu kwa sababu sheria hii ilianzishwa kwa mara ya kwanza dhidi ya Waislamu na dola yao (Dola ya Uthmani) kwenye Mkutano wa Westphalia mwaka 1648, ambao baadaye uligeuka na kuwa Ligi ya Mataifa na kisha Umoja wa Mataifa. Hayo yote si maajabu, lakini cha ajabu ni kwamba watawala wa nchi za Kiislamu jirani na Palestina wanatazama jinai na mauaji yanayoendelea huko huku wakiwa wamenyamaza kimya na kuyazuia majeshi kunusuru (nusrah) Gaza, na kwa hakika Palestina yote. Bali, mbora wao ni yule anayehesabu mashahidi na kuwaita "wafu" na kuwahesabu waliojeruhiwa kana kwamba ni kundi lisilofungamana na upande wowote, bali liko karibu zaidi na Mayahudi, kana kwamba kinachotokea ni katika nchi ya mbali na sio katika Ardhi iliyobarikiwa ambayo Mwenyezi Mungu ameibariki na viunga vyake! Uvamizi wa kikatili wa Mayahudi dhidi ya Gaza haukufanyika siku moja au mbili zilizopita, lakini takriban miezi tisa iliyopita, na watawala wa Kiislamu wamesalia kimya, badala yake, wamehakikisha utekelezwaji wa maazimio ya kimataifa ambayo yalikuwa ni mabaya kwa Waislamu, Mwenyezi Mungu awaangamize, wadanganyika kiasi gani!

**Enyi Majeshi katika Ardhi za Kiislamu:** Je, wakati haujawadia wa damu yenu kuchemka katika mishipa yenu mnapoona na kusikia jinai na mauaji yanayotokea dhidi ya ndugu zenu wa Gaza, na kwa hakika Palestina yote, yanayoathiri watu, miti na mawe?! Je, vilio vya watoto, miito ya wanawake, na maombi ya wazee hayakusukumeni kuwanusuru?

وَإِنِ اسْتَنْصَرُوكُمْ فِي الدِّينِ فَعَلَيْكُمُ النَّصْرُ

**"Lakini wakiomba msaada kwenu katika Dini, basi ni juu yenu kuwasaidia."** [Al-Anfal: 72] Je, Aya za Mwenyezi Mungu Al-Qawi Al-Jabbar (Mwenye nguvu na Mwenye uwezo), hazikusukumini musimame kama waanaume dhidi ya umbile la Kiyahudi?

قَاتِلُوهُمْ يُعَذِّبْهُمُ اللهُ بِأَيْدِيكُمْ وَيُخْزِهِمْ وَيَنْصُرْكُمْ عَلَيْهِمْ وَيَشْفِ صُدُورَ قَوْمٍ مُّؤْمِنِينَ

**"Piganeni nao, Mwenyezi Mungu awaadhibu kwa mikono yenu, na awahizi na akunusuruni muwashinde, na avipoze vifua vya kaumu ya Waumini."** [At-Tawbah: 14] Je, kumtii Mwenyezi Mungu ni bora au ni kuwatii watawala wenu? Wanaofanya usalama wao wa kitaifa kuwa huru na Gaza na watu wake, ilhali ni umbali wa pua na mdomo tu kutoka kwao, au hata chini ya hapo? Hawa ndio watawala wanaowaunga mkono wakoloni makafiri, na wasiwasi wao pekee ni kubakia kwenye viti vyao vya utawala vilivyopinda. Mkiwafuata wao hawatokufaeni duniani wala Akhera, na hoja yenu ya kuwatii itakuwa batili Siku ya Kiyama.

إِذْ تَبَرَّأَ الَّذِينَ اتُّبِعُوا مِنَ الَّذِينَ اتَّبَعُوا وَرَأَوُا الْعَذَابَ وَتَقَطَّعَتْ بِهِمُ الْأَسْبَابُ * وَقَالَ الَّذِينَ اتَّبَعُوا لَوْ أَنَّ لَنَا كَرَّةً فَنَتَبَرَّأَ مِنْهُمْ كَمَا تَبَرَّءُوا مِنَّا كَذَلِكَ يُرِيهِمُ اللهُ أَعْمَالَهُمْ حَسَرَاتٍ عَلَيْهِمْ وَمَا هُمْ بِخَارِجِينَ مِنَ النَّارِ

**"Walio fuatwa watakapo wakataa wale walio wafuata, na hali ya kuwa wamekwisha iona adhabu; na yatakatika mafungamano yao * Na watasema wale walio fuata: Laiti tungeweza kurudi tukawakataa wao kama wanavyo tukataa sisi! Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu atakavyo waonyesha vitendo vyao kuwa majuto yao; wala hawatakuwa wenye kutoka Motoni."** [Al-Baqara: 166-7]

**Enyi Askari katika Majeshi ya Waislamu:** Watu wa umbile la Kiyahudi si watu wa vita au mapigano. Ni waoga na wamekumbwa na udhalilifu na umasikini. Mnashuhudia wanaume waumini kutoka miongoni mwa kaka zenu wakiwa na silaha ambazo hazilinganishwi na silaha za Mayahudi, lakini wanawapiga kwa nguvu, na wale wanaokimbia mbele yao wanakimbilia ndege ili kuwalinda.

لَنْ يَضُرُّوكُمْ إِلَّا أَذًى وَإِنْ يُقَاتِلُوكُمْ يُوَلُّوكُمُ الْأَدْبَارَ ثُمَّ لَا يُنْصَرُونَ

**"Maadui hawatakudhuruni ila ni maudhi tu. Na wakipigana nanyi watakupeni mgongo, na tena hawatanusuriwa."** [Aal-i-Imran: 111] Bila shaka munajua kwamba Palestina ni ardhi iliyobarikiwa... ardhi ya Kiislamu ambayo Mayahudi hawana haki ya kuwa na mamlaka nayo. Hakuna nafasi ya suluhisho la dola mbili ndani yake. Bali itarudi kama vile Al-Farouq alivyoifungua, Makhalifa Waongofu wakailinda, Salah ud-Din akaikomboa, na Abdul Hamid akaihifadhi kutokana na Mayahudi. Itarejea kwa juhudi za askari wakweli wa Mwenyezi Mungu, wale watakaotimiza Hadith ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw), لَتُقَاتِلُنَّ الْيَهُودَ فَلَتَقْتُلُنَّهُمْ.. **"Mtapigana na Mayahudi na mtawaua"** [Imesimuliwa na Muslim kutoka kwa Ibn Umar].

وَلَتَعْلَمُنَّ نَبَأَهُ بَعْدَ حِينٍ

**"Na bila ya shaka mtajua khabari zake baada ya muda."** [Sad: 88]

**H. 6 Dhu al-Hijjah 1445** **Hizb-ut-Tahrir**
**M. : Jumatano, 12 Juni 2024**

Security Council
United Nations

# Marufuku ya Hijab ya Ubelgiji: Kutopendelea upande wowote kama Haki mpya ya Kimungu (Droit Divin)




Mahakama ya Ulaya ya Haki za Kibinadamu (ECHR) imeidhinisha marufuku ya Ubelgiji ya kuvaa hijab shuleni, uamuzi ambao umezusha mijadala kuhusu uhuru wa kidini na usekula barani Ulaya. Mahakama ilipata kwamba marufuku hiyo, iliyokusudiwa kuhakikisha ‘kutopendelea upande wowote’ katika elimu ya umma, haikiuki Mkataba wa Ulaya wa Haki za Kibinadamu. Kesi hiyo ilianzishwa na mwanafunzi mmoja Muislamu ambaye alidai kuwa sera hiyo inakiuka haki zake za uhuru wa dini na elimu. Hata hivyo, ECHR iliamua kwamba marufuku hiyo ilihalalishwa na haja ya kudumisha ‘kutopendelea upande wowote,’ kama ilivyotarajiwa.

Utekelezaji huu wa kibaguzi wa kutoegemea upande wowote ni wa kinafiki. Ingawa hijab, nembo ya kitambulisho cha Muslima, imepigwa marufuku kwa jina la kutoegemea upande wowote, nembo au matendo mengine ya kidini hayakabiliani na kiwango kama hicho cha uchunguzi au marufuku. Kwa mfano, sikukuu na nembo za Kikristo bado zinaweza kuadhimishwa na kuonyeshwa katika muktadha mbalimbali wa umma bila vikwazo sawia. Tofauti hii inafichua kwamba sera hizo hazihusiani na kutoegemea upande wowote na zaidi zinakuhusu kuyalenga makundi maalum ya kidini, Waislamu, kuendeleza aina ya upendeleo na ubaguzi wa kithaqafa. Marufuku hiyo inawaathiri vibaya wanawake wa Kiislamu, ikizidhibiti fursa zao za elimu na machaguo yao ya kibinafsi.

Hijab ina umuhimu mkubwa kwa wanawake wa Kiislamu, ikitumika kama kipengee muhimu cha kitambulisho chao na kujieleza kidini. Kuivaa ni faradhi kutoka kwa Mwenyezi Mungu (swt). Mwenyezi Mungu (swt) asema katika Quran:

**[وَقُل لِّلْمُؤْمِنَاتِ يَغْضُضْنَ مِنْ أَبْصَارِهِنَّ وَيَحْفَظْنَ فُرُوجَهُنَّ وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَلْيَضْرِبْنَ بِخُمُرِهِنَّ عَلَى جُيُوبِهِنَّ وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا لِبُعُولَتِهِن...]**

**“Na waambie Waumini wanawake wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao, wala wasionyeshe uzuri wao isipo kuwa unao dhihirika. Na waangushe shungi zao juu ya vifua vyao, wala wasionyeshe uzuri wao ila kwa waume zao...”** [Al-Nur: 31]

Haishangazi kwamba ECHR ilitoa uamuzi dhidi ya hijab na kuunga mkono marufuku hiyo. Hijab imekuwa ikishambuliwa kwa miaka mingi sasa, ikisifiwa kuwa ni ushamba na ukandamizaji. Ufaransa imefikia hatua ya kupiga marufuku abaya kwa jina la 'kutopendelea upande wowote' ili kulinda "laïcité" (usekula), utengananishaji kanisa na serikali. Kanuni hii iitwayo usekula imeibuka kama mwitikio kwa droit divin (haki ya kimungu), itikadi inayofafanua fikra kwamba mamlaka ya mfalme ya kutawala yamepeanwa moja kwa moja na Mungu, badala ya kuvuliwa kutoka kwa idhini ya watu au ya mfumo wowote wa kisheria wa kisekula.

Hata hivyo, ukweli kwamba ‘kutopendelea upande wowote’ hujadiliwa tu inapohusu Uislamu na mwonekano wa Uislamu katika maeneo ya umma unaonyesha kwamba usekula sio tu umeshindwa kuondoa dhulma ya kimsingi ya haki ya kimungu (droit divin) kutoka Enzi za Kati. Watetezi wake sasa wanatenda sawasawa kabisa na watetezi wa haki ya kimungu katika siku za nyuma. Kwa maana nyengine, sawasawa na wasomi wa zama za kati (medievalists).

Kwa sababu ni kwa nini tunatakiwa kutopendelea upande wowote inapohusu hijab, abaya, swala, Quran na mengine yote yanayohusiana na Uislamu na kitambulisho chetu cha Kiislamu, lakini sio wakati inapohusu sikukuu za Kikristo, upigaji wa kengele za kanisa, kuwepo kwa shule na vyuo vikuu vya Kikatoliki, mitandio ya kichwa ya wanawake wa Kiyahudi, na kippah. Orodha inaendelea na kuendelea.

Hatimaye, shambulizi la hijab, na mwanamke wa Kiislamu kwa jumla, ni shambulizi la moja kwa moja na la kukusudia kwa shakhsia yake ya Kiislamu. Ni shambulizi dhidi ya Uislamu wenyewe.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Sumaya Bint Khayyat**

# HABARI NA MAONI
# Chochote Kinacholevya Ni Tembo Na Kila Tembo Ni Haramu



**Habari:**

Mnamo Mei 22, 2024, kupitia agizo kuu, Gavana wa Mombasa Abdul Swamad Shariff Nassir alipiga marufuku uingiaji, usambazaji, uuzaji na unywaji wa muguka (aina ya kichocheo maarufu kinachojulikana kama Khat au Miraa) au bidhaa zake Mombasa. Agizo sawia na hilo lilitolewa na magavana wa kaunti za Kilifi na Taita Taveta ambao waliapa kukabiliana na uuzaji na matumizi yake. Baadaye, Rais William Ruto alibatilisha marufuku ya kutatanisha iliyowekwa katika baadhi ya maeneo ya nchi. Ulaji wa machipukizi mapya na majani laini yamelaumiwa kwa kuongezeka kwa masuala ya afya ya akili na kuongezeka kwa matatizo ya kijamii, ikiwa ni pamoja na uhalifu.

**Maoni:**

Kupigwa marufuku kwa mogukaa kumeibua hisia kali katika kaunti inayolima muguka ya Embu, huku wakulima na wafanyibiashara wakilaani ilani hiyo ya kufunga biashara kutokana na marufuku hiyo. Hata hivyo, marufuku hiyo imepata uungwaji mkono mkubwa kutoka kwa mashirika ya kidini huku viongozi wa dini ya Kiislamu wakitaka Mugokaa kuainishwa kama dawa za kulevya. Kichocheo hicho ni zao halali chini ya Sheria ya Mazao ya 2013 na Kanuni za Miraa 2023. Rais Ruto amesema Serikali yake imetenga $3.7m (£3m) katika mwaka huu wa kifedha ili kupanua kilimo cha mirungi nchini.

Katika mtazamo wa kisekula na kibepari, hakuna sababu kwa serikali yoyote kupiga marufuku mugokaa na vileo vyote. Maadamu viwanda vya kilimo cha mirungi na vileo vinazingatia sheria, basi vinahimizwa kujitanua ili viweze kuchangia maendeleo ya kiuchumi. Kwa vile ukulima wa Khat na mugokaa ni halali katika nchi hii, basi biashara, pamoja na matumizi yake inaruhusiwa kupanuka kama viwanda vingine mradi tu yazingatie masharti yote ya kisheria yanayohusiana nayo. Ni katika muktadha huu, viongozi kutoka maeneo ya kilimo ya Mugokaa wamelia kwa kupigwa marufuku! Hili linaonyesha kipimo kibovu cha mfumo wa kibepari linapokuja suala la wema na ubaya kwani mfumo huo unazingatia tu faida inayozaa. Hivyo kwa muktadha huu, mugoka ni hatari kwa maisha ya binadamu lakini mfumo wa kibepari unaruhusu kilimo na biashara yake kustawi kwa njia inayowezekana kwa njia rahisi zaidi. Kinyume na Uislamu, mtazamo na kipimo cha matendo ya mwanadamu kinategemea ima halali au haramu. Katika hali hii, ikiwa kitu ni haramu, basi kinaharamishwa kabisa bila kujali manufaa ambayo yanaweza kutoka kwayo.

Wengi wa wanaotafuna mugokaa na kunywa pombe ni miongoni mwa maskini na hata matajiri wanadai kufanya hivyo ili kupunguza msongo wa mawazo. Ingawa sababu hii haihalalishi binadamu mwenye akili timamu kujihusisha na vitendo hivyo, ni kweli kwamba Wakenya wengi maskini hujiingiza katika unywaji wa vileo kama 'njia ya kutoka' kutoka kwa matatizo ya kiuchumi. Hii ni natija ya kutabikishiwa kwao kwa itikadi mbovu ya kibepari yenye mfumo mbovu wa kiuchumi unaotazama tu uzalishaji wa rasilimali na kuzifanya kuishia mikononi mwa watu wachache wenye nguvu hivyo kuwaacha wananchi wengine wakisota kwa umaskini. Uislamu, kwa upande mwingine, umekataza wanadamu kupoteza matumaini ya maisha na mfumo wake wa kiuchumi unahakikisha mgawanyo sahihi na sawa wa rasilimali kwa wote na wengine na kutoruhusu watu wachache tu wenye nguvu kunufaika.

Kwa kumalizia, suluhisho la uovu huu liko katika Uislamu. Uislamu kama itikadi unakataza ulaji au matumizi ya kitu chochote kinachoathiri jamii ya wanadamu kiwe cha kiafya au kijamii. Kwa mujibu wa Uislamu, unywaji wa kilevi chochote yaani vileo ni haram na huhesabiwa kuwa ni miongoni mwa matendo ya Shetani yanayopelekea kuchukiza katika jamii bila kusahau kuwapeleka wanadamu mbali na njia ya haki ya kufuata matamanio. matakwa ya Muumba wetu.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut TahrirKenya**

**JIBU LA SWALI**

# Uhalisia wa Hizb ut Tahrir Baada ya Kusimamishwa Khilafah



**Swali:**

Assalam Alaikum Wa Rahmatullah Wa Barakatuh

Inaelezwa katika Utangulizi wa Rasimu ya Katiba, Kifungu cha 21: Waislamu wana haki ya kuanzisha vyama vya kisiasa ili kuwahisabu watawala, au kufikia madaraka kupitia Ummah.

Swali ni: Ikiwa chama kilicho chukua utawala kilikuwa na mpango wake wa kisiasa, itautabikisha kama ilivyo kwa vyama katika nchi za sasa?

Pia, je ni sahihi kwa Amiri wa chama - kama chama chetu - kushikilia wadhifa wa uongozi wa chama na ule wa khalifa wakati huo huo?

Ikiwa ni sahihi, je chama kinawezaje kumhisabu Khalifa, huku kikiwa chini ya uongozi wa Amiri wake, ambaye ni Khalifa?

Baraka za Mwenyezi Mungu ziwe kwako Amiri wetu, na Mwenyezi Mungu akuruzuku matendo mema.

**Jibu:**

Wa Alaikum Assalam Wa Rahmatullah Wa Barakatuh

Tumetoa swali zaidi ya Jibu la Swali moja juu ya mada hii: mnamo 14/8/1967 na mnamo 26/12/2014, na yana maelezo ya kutosha, kwa hivyo yaregelee.

**Lakini kwa kifupi ni kama ifuatavyo:**

1- Kuchukua utawala wa Hizb ut Tahrir sio kama uchukuaji utawala wa vyama vilivyopo sasa ulimwenguni. Kinachofikia madaraka ni fikra ambayo juu yake chama kimeasisiwa, katika umbo lake la kina, kama ilivyoitabanni, na sio wanachama wa chama. Chama kinafanya kazi kuzileta fikra zake madarakani, sio kuwaleta wanachama wake madarakani.

2- Lakini, kwa kuwa fahamu za hizb haziwezi kutekelezwa vizuri isipokuwa na wale wanaozitabanni na kuishi nazo na kwa ajili yake, hapana budi khalifa awe kutoka kwa hizb, hapana budi wasaidizi wawe kutoka kwa hizb, na hapana budi Amiri wa Jihad awe kutoka kwa hizb. Pande hizi tatu za vyombo vya utawala

*Endelea... UK 8*

hapana budi ziwe kutoka kwa hizb ili fikra itekelezwe na kuhakikisha utekelezaji wake sahihi. Ama kuhusu viungo vyengine vya utawala, vinaweza kuwa kutoka kwa hizb, au vinaweza kuwa kutoka nje ya hizb kwa mujibu wa nguvu na uwezo.

3- Mbali na ukweli kwamba fikra ya hizb kuja madarakani, ni kuwasili kwa hizb madarakani, hizb ni mwangalifu kutowalazimisha wanachama wa hizb kutawala watu na kuchukua tahadhari kubwa dhidi ya hilo. (imesimuliwa kutoka kwa Umar bin Al-Khattab kwamba alipowachagua wanachama wa Baraza la Shura, yaani, wagombea sita wa uongozi wa Khilafah, alikuja kwa Ali na kumwambia: ewe Abu al-Hassan, ikiwa watakupa wewe, usiruhusu Bani Hashim waendelee kutawala watu. Akaja kwa Uthman na kumwambia: Ewe Uthman, ikiwa watakupa (Khilafah), jihadharini na kuwafanya Bani Umayyad waendelea kutawala watu), na ikiwa Khalifa ni kutoka Hizb ut Tahrir, basi wanachama wa hizb watakuwa kwake kama Bani Hashim kwa Ali na Bani Umayyad kwa Uthman, kwa hivyo sio sawa kwake kupitisha uamuzi kwao juu ya watu wengine.

4- Ama kuhusu hizb kumhisabu mtawala pindi chama kinapoingia madarakani, jibu la hilo ni:

Hizb hufanya amali nne: utoaji thaqafa (ya umakinifu na ya jumla), na mvutano wa kifikra katika suala la kufafanua fikra sahihi kutokana na fikra ya batili na fisadi. Amali hizi mbili sio mada ya kuhisabu uwajibikaji, lakini badala yake ni kazi ya kithaqafa na kifikra ya hizb. Kazi ya hizb kufanya yote haya inaendelea, kabla na baada ya utawala, kwani haziathiriwi na kuchukua madaraka ya hizb.

Ama kazi ya tatu (kufichua mipango), sio kazi ya hizb tena kwa sababu uwepo wa hizb madarakani umeondoa suala la chama kinachoonyesha mipango ya kikoloni. Badala yake, inafanywa na vyombo vya serikali, **na kuwahisabu watawala kuwajibika kwa kutabanni maslahi, kama ilivyokuwa kabla ya utawala, inabaki na inafanywa na kamati za Wilayah.**

Kamati za Wilayah, kama ilivyokuwa kabla ya utawala, zina mamlaka ya kuuhisabu uongozi wa chama kuwajibika (Amiri na afisi yake), kwa hivyo wanaendelea kuwa na mamlaka haya ya kuuhisabu uongozi wa chama wakati kiko madarakani, na katika kutabanni maslahi ya Ummah kwa mujibu wa hukmu za Sharia na kuwaangalia kwa wema na ustadi.

Natumai, haya yametosheleza, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi zaidi na Mwingi wa hekima.

**Ndugu Yenu,**
**Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah**

**4 Rabi ul Awal 1445 H**
**19/9/2023 M**